\

# MKATABA WA UPANGAJI WA ENEO

Makubaliano haya ya upangaji wa eneo yamefanyika leo tarehe 01 mwezi 12 mwaka 2023 kati ya ndugu Ndugu FRANCO RICHARD Simu namba +255718863382 wa mtaa wa kisota Kata ya Mji mwema wilaya ya Kigamboni Mkoa wa Dar es salaam, Tanzania mwenye eneo ( **mpangishaji**) kwa upande mwingine.

**Na**

FRANCIS MUGISHA[ MKURUGENZI WA FRANKRIM GROUP LTD] wa Simu namba +255763088945 Mtaa wa Kisota barabara ya dau .wilaya ya kigamboni Dar Es Salaam ambaye ni (**Mpangaji)** kwa upande mmo

**Makubaliano ya Mkataba huu yanashuhudia kama ifuatavyo;**

1. Mwenye eneo amekubali kumpangisha na mpangaji amekubali kupanga eneo lilopo mtaa wa kisota kata mji mwema katika wilaya ya kigamboni .mkoa wa **Dar es salaam.**

2. Mwenye eneo amekubali kumpangisha eneo hilo kwa ajili ya shughuli za biashara na mpangaji amekubali kupanga eneo tajwa.

3. Kwamba mpangaji amekubali kulipa kodi iliyopangwa na mpangishaji kwa mwezi mmoja……………na kodi hii itakuwa ya miezi mitatu mitatu ambapo jumla mpangaji amelipa.150,000/= kiasi ambacho mwenye eneo anakiri kukipokea wakati wa kusaini mkataba huu jumla ni 150,000/= tu.

4. Kwamba, Mkataba huu utakuwa ni kuanzia tarehe 01..Mwezi 12 Mwaka..2023 mpaka tarehe 01.. Mwezi 01 Mwaka 2025

5. Kwamba mkataba huu utaruhusu mpangaji mmoja tu.

6. Kwamba uharibu wowote utakaojitokeza kwenye eneo la mpangaji, mpangaji mwenyewe atawajibika kugharamikia uharibifu huo.

7. Kwamba uendelezaji/uboreshaji wa eneo kwa matakwa na mahitaji ya mpangaji utaweza kufanyika pale ambapo mpangaji atamuhusisha mmliki wa eneo na kupata ridhaa yake.

8. Kwamba, gharama zote za umeme na maji zitakuwa juu ya mpangishwaji/mmliki wa eneo mwenyewe.

9. Kwamba mpangaji hatoruhusiwa wala hatoweza kuvumiliwa endapo atabainika anafanya matendo yoyote yaliyo kinyume cha sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sheria kali zitachukuliwa juu yake pamoja na kulipa fidia pale itakapothibitishwa kufanya vitendo hivyo.

**Kwa ajili hiyo mpangaji anaahidi kwamba;**

a) Atalipa kiasi cha kodi kilichokubaliwa kwenye mkataba huu bila kukosa wala usumbufu.
b) Haruhusiwi kupangisha sehemu yoyote ya eneo aliyopanga bila ruhusa ya mwenye eneo.
c) Atafanya matengenezo ya kitu chochote atakachoharibu katika kipindi cha upangaji.
d) Katika kipindi chote cha upangaji ataiweka eneo katika hali ya usafi.
e) Atarudisha eneo alilopanga kwa mwenye eneo mara baada ya mkataba huu kuisha ikiwa katika hali nzuri.
f) Atalipa kodi ya eneo kwa wakati /muda na kipindi kilichopangwa bila kukosa.
g) Eneo lililopangishwa ni kwa ajili ya matumizi ya biashara tu.

**MWENYE ENEO** anakubaliana na mpangaji kwamba iwapo mpangaji atalipa kodi kama ilivyokubalika na kutimiza masharti yote katika mkataba huu, basi atafanya biashara na kukaa kwenye sehemu aliyopanga bila bugudha yoyote toka kwa mwenye Eneo au mtu yoyote kwa niaba ya mwenye eneo [kiwanja]

**ISIPOKUWA** pande zote mbili zinakubaliana kwamba;

i. Iwapo mpangaji atavunja ama kushindwa kutimiza mojawapo ya masharti ya mkataba huu, mwenye eneo atakuwa na haki ya kuvunja mkataba huu bila kuathiri haki zake nyingine alizonazo mbele ya sheria.

ii. Mkataba huu ni wa muda wa miezi mitatu (3) ila unaweza kuendelezwa (renewal) utakapoisha kwa makubaliano ya pande mbili.
iii. Mwenye eneo atawajibika kutoa taarifa ya mwezi mmoja kabla ya kuamua kumtoa mpangaji yeyote pale atakapoona anahitaji kumtoa kwenye eneo aliyompangisha.
iv. Kwamba mpangishaji anamhakikishia kuwa eneo hilo halina matatizo yoyote.

Kwa ushuhuda huu wahusika wanaweka saini zao,kwenye mkataba huu kama ifuatavyo:

Imetiwa saini na
Kutolewa na mtajwa
..................................
leo tarehe 01..Mwezi 12..Mwaka 2023

.....................
**MPANGISHAJI**

**Shahidi wa Mpangishaji**
Jina... MAGRETH RICHARD
Sifa... MMILIKI - PADO
Simu... +255718863382
Kazi..............................
Makazi... KISOTA
Tarehe... 01/12/2023
Sahihi..............................

FRANKRIM GROUP LIMITED P. O. Box 9976 DAR ES SALAAM

Imetiwa saini na kutolewa
.........................................
Leo tarehe ....Mwezi ...Mwaka.........

.....................
**MPANGAJI**

**Shahidi wa Mpangaji**
Jina... PETRONILA MUGISHA
Sifa... MKURUGENZI - TETOTO
Simu... +255763088945
Kazi..............................
Makazi... KISOTA
Tarehe... 01/12/2023
Sahihi..............................

**MBELE YANGU :**

JINA... RITA NIBWO NTAGAZWA
SAHIHI.............................
ANUANI... S.L.P 23164
TAREHE... 01/12/2023
WADHIFA: KAMISHINA WA VIAPO

Rita Nibwo Ntagazwa Box 23164 Dar es Salaam Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths